

HALMASHAURI YA WILAYA YA MKURANGA
Barua zote ziandikwe kwa: Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,



Simu Na 023 2402738,
Fax Na 023 402706
Unapojibu tafadhali taja:

S.L.P. 10,
MKURANGA,
PWANI.

Kumb. Na. MDC/L.20/6/VOL.LXX/93

10/2/2021

Mkurugenzi Mkuu,
Kituo cha Uwekezaji Tanzania,
S.L.P.938,
Dar es salaam

**YAH: KAMPUNI YA UWEKEZAJI YA ECO PLASTICS LIMITED KIWANJA
NA.29 NA KAMAKA IT LIMITED KIWANJA NA 30 KITALU B, WILAYANI
MKURANGA**

Rejea mada tajwa hapo juu.

Ninakujulisha kwamba, viwanja tajwa hapo juu vimetokana na kurejeshwa kwa miliki na baadae kufutwa kwa upimaji wa viwanja **Na.1-3 Kitalu B Kisemvule**, ambapo upangaji na upimaji upya wa eneo lenye viwanja tajwa umezalisha viwanja **Na. 25-30 Kitalu B Kisemvule**.


Kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999, fungu la 19-20 na Sheria ya Uwekezaji Tanzania Na.26 ya mwaka 1997, aidha kwa kuzingatia fungu la 12 na 179 Sheria ya Ardhi Na.4 ya mwaka 1999 na Tangazo la Serikali Na.72 la tarehe 4/5/2001, kanuni za Ardhi za 2001, kanuni ya 9C(v), kiwanja hiki kinatakiwa kuwa miliki ya Kituo cha Uwekezaji Tanzania.

Halmashauri ya Wilaya inazitambulisha Kampuni hizi kutoka nje ya nchi kwako ili ziweze kupatiwa Certificate of Incentive zenye kuonyesha namba ya kiwanja uwekezaji utakapofanyika ili kuiwezesha Halmashauri ya Wilaya kuandaa **Designation for Investment-Land form Na.1** ili viwanja hivi vitangazwe kuwa vya Uwekezaji na hatimaye kuingizwa katika **kamati ya Ugawaji wa Ardhi Taifa**.

Kiwanja Na.25-30 Kitalu B Kisemvule kimetokana na kurejeshwa kwa hati miliki na kufutwa kwa upimaji kwa umiliki wa Kiwanja Na.1-3 Kitalu B Kisemvule baada ya **Lodhia Steel Industries Limited** kuuza vipande vya Ardhi ndani ya miliki hii kabla ya kugawanywa katika Mipango Miji na baadae kupimwa na kusajili viwanja vipya **Na.25-30 Kitalu B Kisemvule**, ambavyo sasa (**kiwanja Na.25-27-Lodhia Steel Industries Limited**, **kiwanja Na. 28-Ak-An Wood Limited**, **Kiwanja Na.29-Eco Plastics Limited** na **kiwanja Na. 30- Kamaka IT Limited**)

Nawasilisha kwako kwa hatua zaidi, nimeambatanisha nyaraka muhimu kwa urahisi wa rejea (**Taarifa ya kurjesha viwanja hivi ofisi ya Kamishna wa Ardhi, Hati ya urejesho wa Miliki na Ramani ya upimaji**).

Kwa hatua zako muhimu.



Chagiye R.M
Kny.Mkurugenzi Mtendaji (W),
Mkuranga.

Nakala: **Mkurugenzi Mtendaji (W)**
Mkuranga -Kwa taarifa

Eco Plastics Limited
Dar es salaam -Fuatilia nyaraka husika TIC

Kamaka IT Limited
Dar es salaam -Fuatilia nyaraka husika TIC